

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA

SIMU: MKURUGENZI WA MANISPAA  
+ 255 736 200910  
OFISI ZOTE: +255 736 200911/12  
FAX: +255 028 736 200910  
E-mail: md@ilemelamc.go.tz



S.L.P 735,  
MWANZA  
24/08/2022

## TANGAZO LA UZAJI WA VIWANJA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA HALMASHAURI INAUZA VIWANJA VILIVYOPIMWA KWA MATUMIZI MBALIMBALI KUPITIA MRADI WAKE WA KUPANGA, KUPIMA NA KUMILIKISHA ARDHI.

VIWANJA HIVYO VINAPATIKANA NDANI YA MJI MPYA NA WAKISASA KATIKA KATA YA SANGABUYE KANDO YA BARABARA KUU ITOKAYO UWANJA WA NDEGE MWANZA KUELEKEA KAYENZE NA KANDO YA ZIWA VICTORIA. ENEO HILI LIPO TAKRIBANI KILOMITA KUMI NA TATU (13) KUTOKA MAKAO MAKUU YA MANISPAA YA ILEMELA; KILOMITATISA (9) KUTOKA UWANJA WA NDEGE MWANZA NA KILOMITA TATU (3) KUTOKA ILIPOJENGWA HOSPITALI YA WILAYA YA ILEMELA. BEI YA VIWANJA HIVI NI KAMA IFUATAVYO:-


Na.	MATUMIZI YA KIWANJA	BEI YA KILA MITA MOJA YA MRABA (TSHS)
1.	VIWANJA VYA FUKWE (BEACH PLOT)	30,000/=
2.	MAKAZI BLOCK LA PILI BAADA YA FUKWE	20,000/=
3.	MAKAZI (BLOCK LA TATU KUTOKA BEACH)	8,000/=
4.	VIWANJA KANDO YA BARABARA KUU (BIASHARA)	6,000/=
5.	MAKAZI	4,500/=
6.	TAASISI (Shule, Zahanati, Sehemu za kuabudia)	4,500/=
7.	MASHAMBA MJINI, VIWANDA VIDOGO	4,500/=

FOMU ZA MAOMBI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA MAKAO MAKUU YA MANISPAA KWA BEI YA TSHS.20,000/= FOMU ZINATOLEWA NDANI YA WIKI MBILI KUENZIA SIKU YA JUMATANO TAREHE 24 AGOSTI, 2022. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 07 SEPTEMBER, 2022 FOMU ZIREJESHWE NDANI YA SIKU ZA KAZI KUENZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.

UKICHUKUA FOMU UNAHAKIKISHIWA KUPATA KIWANJA NA UTATAKIWA KULIPA NUSU YA GHARAMA YA KIWANJA HICHO NDANI YA SIKU SABA NA KIASI KINACHOBAKI KITALIPWA NDANI YA SIKU SITINI (60) TOKA SIKU YA MALIPO YA AWALI BILA KUPITILIZA. ENDAPO MALIPO HAYO HAYATAKAMILISHWA KWA WAKATI MALIPO YALIYOTANGULIZWA HAYATARESHWA NA KIWANJA KITAGAWIWA KWA MWOMBAJI MWINGINE BILA KUTOA TAARIFA YOYOTE.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA SIMU NA 0787-737616, 0755-370460 NA 0755-328651.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA

  
ENG. MODEST J. APOLINARY,  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
ILEMELA.

